


malaria



haikubaliki

PEACE CORPS 2015



Omar na Juma ni marafiki sana. Hucheza pamoja kila siku. Siku moja, Juma alikuja shuleni na hakuweza kumwona Omar.


“Omar yuko wapi?” Juma alimwuliza mwalimu.

Mwalimu alijibu “Omar anaumwa sana. Ana malaria kali. Yuko hospitali.”



Hili kuwa habari mbaya sana. Juma hakuweza kusikiliza au kusoma. Alimwamba mwalimu anaumwa na Juma alirudi nyumbani kwao. Juma na kaka yake walienda hospitalini kumtembelea Omar.


Hospitali



Walifika hospitalini na walimwona Omar. Omar alionekana na umwa sana na alilala kitandani. Alikuwa macho lakini alichoka sana. Walisalamiana, halafu Omar alilala fofoto.

Juma alimwuliza daktari "Omar atapona?"

Daktari alijibu "Mungu anajua mwenyewe. Omar ana homa kali, kutapika, degedege, na kuhisi baridi. Labda atapona. Labda atakufa."




Juma alihuzanika. Alikaa hospitalini siku nzima. Halafu, alirudi hospitali kila siku. Baada ya siku chache, Omar alianza kupona na Juma na Omar walizungumza.

Juma alifurahi Omar aliendelea kupona lakini Juma aliuliza “Vipi ulipata malaria? Ulilala kwenye chandarua kila usiku, au siyo?”

“Hapana,” Omar alijibu, “Nimesahau kulala kwenye chandarua.”

“Kweli? Umesahau?” Juma aliuliza, “Lakini ulienda haraka zahanati kupima baada ya homa, au siyo?”


“Hapana,” Omar alijibu, “Nilifikiri naweza kupona bila dawa.”



“Ulisahau elimu ya mwalimu wa afya?” Juma aliuliza. “Alisema Lala Kwenye Chandarua Kila Usiku na Kama Una Homa, Nenda Zahanati Haraka Kadiri Iwezakanavyo Kupima!”

“Kama unge viyu hivi, usunge pata malaria kali.”

Aa Bb Cc



“Sasa,” Juma aliendelea kusema, “tulikosekana shuleni. Kama hatutapata elimu nzuri, hatutapata kazi nzuri na hela nyingi ya baadaye. Ninataka hela nyingi na afya nzuri! Sijui wewe.”

“Hata Mimi,” Omar alisema. “Tafadhali niwie radhi. Nitalala kwenye chandarua kila usiku na nitaenda zahanati nikipata dalili za malaria kama: homa, kutapika, kuhisi baridi, kuharisha, au kuumwa sana ya kichwa.”



Siku zilizifuata, Omar na Juma walirudi shuleni na walifurahi kuendelea na elimu yao. Halafu, walicheza mpira wa miguu na Omar alisema "Tukiendelea tutakuwa na afya nzuri, labda tutacheza mpira kwenye Timu ya Yanga au Simba ya baadaye!"